# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS TANZANIA

Toleo No. 93
Novemba - Desemba 2020


## SIMULIZI LA WINDA: KUKATAA UKEKETAJI



UNFPA inasaidia juhudi za kuharakisha maendeleo kuelekea katika kutokuwa kabisa na ukeketaji ifikapo mwaka 2030 na kuwepo kwa dunia iliyo bora na yenye usawa zaidi kwa wasichana kama Winda. ***Picha: UNFPA Tanzania***

## VIDOKEZO


- Vijana wawashawishi Wabunge juu ya ajenda yao ya mabadiliko
- Watoto mapacha wakimbizi wawa miongoni mwa waliopata vyeti vya kuzaliwa vya Tanzania
- SIDO: Mabadiliko ya mahali baada ya uwekezaji
- Kinga ya magonjwa: Watumishi wote wa mipakani wawe na tahadhari


Winda* alikuwa na umri wa miaka 13 na alikuwa tayari kujiunga na elimu ya sekondari pale baba yake alipomtaka kwenda kufanyiwa ukeketaji. “Aliniambia kuwa sasa nimekua na kwamba ilikuwa ni lazima nifanyiwe ukeketaji ili familia yangu ijivunie nami na kupata heshima katika jamii,” anakumbuka.

Huku madhara ya ukeketaji yakiwa yanajulikana waziwazi inaweza kuonekana kama vile ni jambo jepesi kusema hapana kwa ukeketaji. Lakini kwa upande wa Winda na mamilioni ya wanawake na wasichana kote duniani wanaoishi katika jamii ambako ukeketaji unaonekana kama hatua muhimu katika safari ya kukua na ambako wasichana wasiokeketwa wananyanyapaliwa na mara nyingi hawawezi kuolewa kukataa kukeketwa maana yke ni kupoteza jamii yako, familia yako na marafiki zako.

Ukeketaji ni kitendo kilichoharamishwa nchini Tanzania tangu mwaka 1998 na serikali imekuwa ikifanya kila juhudi kukomesha vitendo hivyo, kam inavyoelezwa katika ajenda za maendeleo za kitaifa, kikanda na dunia, na kama inavyoshuhudiwa na kupungua kwa vitendo hivyo nchini. Hata hivyo, bado kuna tofauti kutoka mkoa mmoja hadi mwingine ambapo Mkoa wa Mara alikozaliwa Winda asilimia 32 ya wanawake wenye miaka 15 hadi 49 bado wanakeketwa.

Winda alipata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji baada ya wanaharakati wa kukomesha ukeketaji

***Inaendelea Ukurasa wa 2***

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa 1*

kutembelea shuleni alikokuwa akisoma. Alijua kwamba endapo angalifanyiwa ukeketaji basi angalipatwa na madhara ya muda mfupi na muda mrefu, au hata kifo, na hayo yalimwogofya sana. Aliwambembeleza wanafamilia yake wasimfanyie ukeketaji ambapo aliungwa mkono na kaka yake lakini walikataa katakata kumsikiliza.

Winda alifanya uamuzi wa kishujaa na kutoroka nyumbani kwao ambapo alitembea kwa siku tatu hadi Kituo cha Polisi cha Mugumu. Hapo alikutana na Sijari, askari polisi anayeshughulikia Dawati la Jinsia na Watoto, ambaye alimpeleka Winda katika makazi salama chini ya taasisi ya Hope for Women and Girls, Tanzania, (Matumaini kwa Wanawake na Wasichana) huko Serengeti. Hivi sasa Winda ana umri wa miaka 17 na bado anaishi katika makazi hayo salama. Anapata msaada wa kieleimu na anasema ndoto yake ni kuwa daktari.

Winda ni miongoni mwa wanawake vijana wengi wanaokataa ukeketaji nchini Tanzania, na hayuko peke yake. Vijana, wazazi na jamii wamefanya uamuzi kwamba hawataki kuendelea vitendo hivyo ya ukeketaji, kwamba wanapenda watoto wao wawe na hatma njema maishani dunia iliyo bora zaidi na yenye usawa kwa binti zao.

UNFPA imedhamiria kuendelea kuongeza juhudi za kufikia lengo la kukomesha ukeketaji ifikapo mwaka 2030 kuanzia kuimarisha mazingira ya sera nchini Tanzania hadi kuvuka mipaka katika kuimarisha mifumo ya kinga na utoaji mwitikio; kuongeza utoaji elimu katika jamii na shule na kupanua taratibu nyingine za hatua za makuzi ya mtu.

Tunapoelekea katika Siku ya Kimataifa ya Kutovumilia Kabisa kwa wasichana kama Winda na wengineo wengi kama yeye tunatoa wito unaorindika kote duniani: "Huu si wakati wa kutochukua hatua: Unganeni, toeni fedha na chukueni hatua kukomesha ukeketaji".

## SIKU YA UKIMWI DUNIANI 2020: KUTUMIA UBUNIFU KATIKA HUDUMA ZA VVU ILI KUPANUA NA KUHAKIKISHA MATUNZO ENDELEVU YA VVU

Dunia imepiga hatua kubwa tangu miaka ya mwisho ya 1990, lakini tatizo la VVU bado ni kubwa katika masuala ya afya ya jamii. Na kama ilivyo kwa masuala mengine makubwa ya afya ya jamii, titizo hili linaongeza changamoto ya ziada katika kipindi cha janga la COVID-19.

Mnamo Desemba Mosi, mashirika ya Umoja wa Mataifa ya WHO, UNAIDS, UNESCO na UNICEF yaliungana na Serikali ya Tanzania, washirika, watekelezaji wa programu, vyama vya kiraia na jamii kuwakumbuka wale wanaotoa huduma za VVU, na katika kutoa wito kwa viongozi wa dunia na wananchi kuungana kwa ajili ya "umoja wa kidunia" ili kudumisha huduma muhimu za VVU katika kipindi cha janga la COVID-19 na baada ya hapo. Ni wito wa kuwekea mkazo makundi yaliyo hatarini na kupanua utoaji wa huduma kwa watoto na vijana walio katika umri wa balehe.

Waziri Mkuu, Mh. Kassim Majaliwa, alikuwa mgeni rasmi katika maadhimisho yaliyofanyika Mkoa wa Kilimanjaro na kusema kwa masikitiko kuwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24 ndiyo wanaochangia asilimia 80 ya maambukizi mapya. Viwango vya juu vya maambukizi miongoni mwa vijana ni changamoto kubwa katika juhudi za Tanzania za kupiga hatua katika Malengo ya

*Inaendelea Ukurasa wa 3*

*Kutoka ukurasa wa 2*

Maendeleo Endelevu katika afya, ambayo yanalenga kupunguza maambukizi mpaya katika jamii, wakiwemo vijana.

Kazi ya Umoja wa Mataifa ya kupambana na VVU/UKIMWI nchini Tanzania imekazia katika utungaji sera na kutoa miongozo inayolenga kupunguza ongezeko la maambukizi mapya na kuhakikisha upatikanaji wa dawa a kufubaza virusi (ARVs) kwa watoto, vijana wa umri wa balehe na watu wazima wanaoishi na VVU.

Umoja wa Mataifa, kwa kushirikiana na washirika wake, imeisaidia Tanzania kuandaa mwongozo wa Kujipima VVU (HIV ST) kama mkakati wa nyongeza wa kupima VVU katika makundi mbalimbali ya jamii. Mwongozo huo umetumika kama msingi wa kuoanisha fedha na uombaji fedha katika Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa kipindi cha 2021-2023.

Katika mwaka 2020, Umoja wa Mataifa umekuwa na mchango mkubwa katika kusaidia tafsiri ya Mpango wa Uharakishaji Huduma za Upimaji VVU (Accelerated Plan for HTS) katika ngazi za mikoa na za chini zaidi ambako mikoa tisa yenye mzigo mkubwa wa VVU ilisaidiwa kuandaa mipango ya utekelezaji kwa ajili ya ukaziaji, ulengaji na utoaji kipaumbele kwa upimaji wa VVU kwa kuzingatia mzigo wa ugonjwa.

Kwa upande wake, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic, alirejea ahadi ya Umoja wa Mataifa wa kumaliza kabisa UKIMWI. "Umoja wa Mataifa unashirikiana kwa karibu na Serikali kwa lengo la pamoja la kuhakikisha kunakuwa na ugawaji ulio sawa wa mafanikio ya maendeleo katika nchi nzima, na kukomesha janga la UKIMWI ifikapo mwaka 2030, jambo ambalo litakuwa na athari chanya kwa watu wa Tanzania," alisema.




Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa, Zlatan Milisic (kushoto), akimkaribisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kulia) katika Banda la Umoja wa Mataifa katika maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani katika Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Bw. Milisic alirejea ahadi ya Umoja wa Mataifa ya kuisadia Serikali ya Tanzania kupambana na VVU/UKIMWI. ***Picha: Deborah Kaluzi/UN Tanzania***

# WATOTO MAPACHA WAKIMBIZI WAWA MIONGONI MWA WALIOPATA VYETI VYA KUZALIWA VYA TANZANIA




Zeomary na mapacha wake wakiwa katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta katika Wilaya ya Kibondo, Mkoa wa Kigoma. *Picha: Maimuna Mtengela/ UNHCR Tanzania*

Wakati Zeomary Rudashi akifanya haraka kuelekea katika kituo cha usajili kilicho katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta nchini Tanzania, furaha yake haielezeki. Leo ni siku ya kipekee, si joto la jua wala nini kinachoweza kumwondelea furaha yake.

Anainama kidogo ili kumweka sawa mmoja wa watoto wake mapacha, aliyefungwa vizuri kwa mbeleko mgongoni kwake na kisha anamhimiza binti yake mwenye umri wa miaka saba aliyembeba mtoto pacha mwingine.

"Leo ni siku kubwa kwa Belyce na Jaqueline ambao ndio kwanza wana wiki tatu tangu wazaliwe," anasema huku akitabasamu wakati akijiunga kwenye mstari ili kupata huduma. "Watapata vyeti vya kuzaliwa. Sasa ninajihisi kama kuna mahali ambako wanapaita nyumbani."

Zeomary, ambaye ni mkimbizi kutoka Burundi, ni mama wa watoto saba na amekuwa akiishi katika Kambi ya Nduta kwa miaka mitano sasa. Alikimbia Burundi baada ya machafuko ya kisiasa ya mwaka 2015, na kutafuta usalama nchini Tanzania. Kwa kuwa aliacha mali na nyaraka zote muhimu za familia yake kwao, daima huwa na mashaka ikiwa watoto wake watatambuliwa kama raia wa Burundi wasije kuishia kuwa watu wasio na nchi.

Lakini kwa sababu kuna mpango wa kusajili vizazi, unaosimamiwa na Wakawa wa Usajili wa Vizazi na Vifo na Nyaraka Mbalimbali (RITA), Wizara ya Mambo ya Ndani, Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Baraza la Wakimbizi la Norwaya na wadau wengine, watoto watatu wa Zumary waliozaliwa nchini Tanzania watapata vyeti vyao vya kuzaliwa, pamoja na watoto wengine 13,500 wa wakimbizi walio na umri chini

*Inaendelea Ukurasa wa 5*

*Kutoka ukurasa wa 4*

ya miaka mitano. Hii n mara ya kwanza ambapo utaratibu huu unawajumuisha watoto kama wa Zumary.

Kampeni ya #IBelong (inayoweza kutafsiriwa kama 'Nina Kwetu') inalenga kukomesha hali ya kutokuwa na uraia ifikapo mwaka 2024 na tayari kampeni hiyo inatimiza miaka sita mwaka huu. Viongozi wa dunia wanaaswa kuwajumuisha na kuwalinda watu wasio na uraia na kufanya maamuzi mazito na ya haraka ya kufutilia mbali ukosefu wa uraia.

Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania, Antonio Jose Canhandula, ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa hatua ya kuwajumuisha wakimbizi katika juhudi hizi. "Haki ya kupata jina, utambulisho na kizazi kusajiliwa ni haki ya watoto waote," alisema. "Hatua hii chanya itawapatia ulinzi muhimu wa kisheria."

Aliongeza kusema kwamba wakati ambapo ukosefu wa usajili wa uzazi si jambo linalomnyima mtoto uraia, kutokuwepo kwake kunaweza kuwa kikwazo cha watu kudhitibisha asili na mahali walikozaliwa, ambavyo ni vipengele muhimu katika kuthibitisha haii ya uraia katika Dola.

Zoezi la usajili, ambalo lilifanyika katika Kambi ya Nduta kama majaribio, litaenea pia katika kambi za Mtendeli na Nyarugusu. Kwa ujumla, watoto 55,000 hawana vyeti vya kuzaliwa na hivyo hawa watanufaika. "Mapacha wangu wenye bahati wamekuja na neema katika jamii. Yaani, nina hamu nifike nyumbani haraka nimwonyeshe mume wangu vyeti hivi," anasema kwa furaha.



Zeomary akiwa katika mchakato wa kusajili vyeti vya kuzaliwa. ***Picha: Maimuna Mtengela/ UNHCR Tanzania***

# VIJANA WAWASHAWISHI WABUNGE JUU YA AJENDA YAO YA MABADILIKO



“Kama kijana, tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba mifumo ya maji katika shule zetu na nchini kwetu inaendelezwa ili watoto walindwe dhidi ya magonjwa ya kuambukiza. Watoto wanaweza pia kuwa mashujaa wa Usafi wa Mazingra na Maji (WASH)!”- Rose Mweleka, Kijana Kinara wa UNICEF na Mhitimu wa Chuo Kikuu anasema wakati akihutubia Wabunge.

***All Photos Credit: UNICEF Tanzania***

Mnamo Novemba 20, 2020, vijana nchini Tanzania waliadhimisha Siku ya Mtoto Duniani pamoja na zaidi ya Wabunge 300 waliochaguliwa ambapo waliwakabidhi wawakilishi hao wa watu Ajenda yao ya mabadiliko, wakiwaasa kuweka kipaumbele masuala muhimu kama vile elimu, usafi na mazingira (WASH) na ulinzi wa mtoto ili kuimarisha ustawi wa watoto nchini.

Watetezi vijana Abdullatif Hassan (16), Agape Joster (13), Rose Mweleka (24) na Mariam Mbaga (26) waliwasilisha mapendekezo makuu kutoka katika Ajenda ya Watoto na vijana iliandaliwa kwa mashauriano na zaidi ya watoto 34,000 mwaka 2019 kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 30 ya Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC@30). Zaidi ya watoto milioni 5 walifikiwa kwa ujumbe kuhusu CRC na haki zao kama sehemu ya maandalizi ya Ajenda iliyozinduliwa na Rais Mstaafu Mh. Ali Hassan Mwinyi.

Tukio hilo lililoandaliwa chini ya ujumbe: ‘Reimagine a Better World for Every Child,’ yaani ‘Fikiria Upya kuhusu Dunia Bora zaidi kwa Kila Mtoto’, lilifanyika Jijini Dodoma ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Spika wa Bunge la Jamhuri, Mh. Job Ndugai. Wengine waliohudhuria ni pamoja na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri, Mh. Dkt. Tulia Ackson, ambaye alitoa ahadi nzito zitakazofungua milango kwa mazungumzo ya kimkakati kwa ajili ya siku zijazo. “Tumewasikia. Sisi kama Wabunge, tunaelewa kuwa tuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha tunajadiliana masuala yanayowaathiri watoto wetu na kuisukuma serikali kuchukua hatua zinazostahiki za kukabiliana na yote hayo. Tunaahidi kuiutumia ajenda ambayo mmeiwasilisha kwetu na tutaitumia kama rejea yetu tunaposukuma masuala muhimu mliyoyapendekeza,” alisema Mh. Ndugai.

Katika maelezo yake, Mratibu

*Inaendelea Ukurasa wa 7*

*Kutoka ukurasa wa 6*


wa Umoja wa Mataifa nchini

Tanzania, Bw. Zlatan Milisic, alisisitiza kwamba ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu mwaka 2030, ni lazima kuwela maslahi ya watoto mbele katika ajenda. “Tafsiri ya Maendeleo endelevu ni maendeleo yanayoweza kuendelezwa katika vizazi vijavyo. Kwa hiyo, kufanya maamuzi sahihi kwa ajili ya watoto ni suala muhimu katika utekelezaji wa ajenda ya SDG.”




“Wabunge wana mamlaka ya kuandaa dira ya nchi na kusimamia maendeleo yake. Maamumzi mnayofanya hapa leo yanaweza kuathiri moja kwa moja jinsi gani watoto wataendelezwa katika siku zijazo. Tunawaomba kutumia mamlaka hayo na kuwaweka watoto kwanza!” - Shalini Bahuguna, Mwakilishi wa UNICEF Tanzania, akizungumza katika siku ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto Duniani (WCD).

Kwa upande wake, Mwakilishi wa UNICEF nchini Tanzania, Bi. Shalini Bahuguna, alisema SDGs yatafikiwa tu ikiwa sote tutashirikiana na kuweka upya ahadi zetu kwa kuzingatia kanauni na utekelezajiwa CRC. “Kama Wabunge, mna wajibu muhimu wa kusaidia kufikiwa kwa malengo ya SDG. Mnaweza kutunga sera madhubuti na kujadili, na kutunga sheria zinazowalinda watoto na kusimamia utekelezaji wake katika majimbo yenu. Mnaweza pia kuzungumza kwa niaba ya watoto pale mnapoelewa masuala yanayoathiri ustawi wao na kuanzisha mijadala na kuchukua hatua kupitia sera, sheria na uwekezaji wenye tijia kwa manufaa ya watoto,” aliongeza.



Kabla ya Maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani, Bunge la Tanzania lilingarishwa kwa rangi ya bluu ya UNICEF Tanzania kuonyesha kuunga mkono na ahadi ya kulinda haki za mtoto nchini. Kung’arisha kwa rangi ya bluu katika Siku ya Watoto Duniani ni ishara ya jukumu la UNICEF la kusimamia haki za kila mtoto na kupigania kuleta dunia bora zaidi kwa kila mtoto.



Maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani yalifanyika mkoani Dodoma ambapo mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Job Ndugai, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika siku hii Wabunge walisikiliza sauti za vijana na kuungana na UNICEF katika kufikiria hatima bora ya watoto wa Tanzania.

*Inaendelea Ukurasa wa 8*

*Kutoka ukurasa wa 7*




"Waheshimiwa Wabunge, ninawaasa kusoma Ajenda ya Watoto. Sikilizeni yale wanayosema watoto hawa. Tuna wajibu wa kuchukua mapendekezo yao na kuyageuza kupata uhalisia na kujenga hatima njema ya kila mtoto wa Tanzania," - Mh. Job Ndugai, Spika wa Bunge la Muungano.




Katika Maadhimisho ya Siku ya Watoto Duniani, Vinara wa UNICEF na Wabunge walisherehekea siku hii ya kipekee Bungeni na kutoa ahadi ya kuendeleza haki za watoto na pia kutimiza haki za kila mtoto.

# MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI YAFANA ZANZIBAR




Mgeni Rasmi, Mh. Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar akiwasalimia baadhi ya waandaaji (UNAIDS na ZAC) wa maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani (WAD) nje ya Ukumbi wa Idris Abdul Wakil. ***Picha: Agnes Kenneth/UN Tanzania***

Desemba Mosi kila mwaka, dunia hufanya kumbukumbu za Siku ya UKIMWI Duniani. Watu kote ulimwenguni huungana ili kuonyesha uungaji mkono wao watu wanaoishi na walioathirika na VVU na kuwakumbuka wale waliopoteza maisha yao kwa sababu ya UKIMWI. Kwa upande wa Zanzibar, kumbukumbu hizo zilifanyika katika Ukumbi wa Idris Abdul Wakil ambako viongozi wa serikali na washirika wa maendeleo walishirikiana ili kuadhimisha mafanikio yaliyokwishapatikana na kurejea upya ahadi zao za kukomesha UKIMWI huko Zanzibar. Kumbukumbu hizo zilizodumu kwa juma moja na siku ya kilele zilifanikishwa na UNAIDS, UNICEF, UNFPA na AMREF Africa, ambapo mgeni rasmi alikuwa Mh. Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Ni muhimu kutambua kwamba, kwa upande wa data kwa ujumla, Zanzibar iko katika mwelekeo sahihi wa kufikia malengo yake ya 90-90-90 hadi mwishoni mwa mwaka huu. Hadi sasa data zinaonyesha kuna mafanikio kwa kiwango cha 90-93-95, ambapo programu ya taifa inafanya kazi ya kuchambua mafanikio haya ili kupata data zenye mnyumbuliko zaidi zitakazosaidia kubaini paliko na upungufu na kufanyiwa kazi katika makundi rika yote, hasa wale walio hatarini zaidi na ambao kuna uwezekano wa kubakizwa nyuma.

Mwenyekiti wa Tume ya UKIMWI ya Zanzibar (ZAC), Dkt. Salhia Ali Muhsin, alitoa wito kwa serikali na washirika kuongeza msaada na fedha katika miradi inayolenga kumaliza VVU/UKIMWI nchini. Vilevile, alipendekeza kwamba ni muhimu kuwepo na udhibiti zaidi katika matumizi ya mitandao ya kijamii, hasa kwa vijana.

Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, Dkt. Loy George, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha mshikamano na kila mmoja kutimiza wajibu wake ili kukomesha UKIMWI huko Zanzibar. Aliiasa serikali na washirika wote kusaidia uwekjamii nchini na masuala mengine yaliyo muhimu ili kukomesha UKIMWI ifikapo mwaka 2030.

Mh. Hemed Suleiman Abdalla alisisitiza juu ya ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi ili kumaliza UKIMWI katika jamii yetu. Kwa kuongezea, aliwashukuru washirika wote kwa michango yao mbalimbali katika kusaidia juhudi za Zanzibar katika kukabiliana na UKIMWI.

*Inaendelea Ukurasa wa 10*

*Kutoka ukurasa wa 9*



Mgeni Rasmi, Mh. Hemed Suleiman Abdulla, Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar akiwasalimia baadhi ya waandaaji (UNAIDS na ZAC) wa maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani (WAD) nje ya Ukumbi wa Idris Abdul Wakil. ***Picha: Agnes Kenneth/UN Tanzania***



Washiriki katika maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani huko Zanzibar, wakiwemo wawakilishi wa Serikali na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. ***Picha: Agnes Kenneth/ UN Tanzania***

# JUHUDI ZA KUHAMASISHA BIASHARA YA MPAKANI



Justina Amato, mwuza nyanya katika Soko la Mpakani la Muhange, Kakonko, Kigoma. ***Picha: UNCDF Tanzania***

Soko la mpakani la Muhange liko umbali wa kilometa 46 upande wa magharibi wa mji wa Kakonko katika mpaka na nchi jirani ya Jamhuri ya Burundi. Kwa miaka mingi soko hili limewavutia wafanyabiashara kutoka katika maeneo ya jirani ikiwemo eneo la ndani linalokwenda hadi kilomita 200 katika kila nchi. Bidhaa na huduma zinazopatikana ni pamoja na mifugo, kuku, nafaka, bidhaa za matunda na mbogamboga, vifaa vya ujenzi, nguo, vyakula na vinywaji. Kupitia Mpango wa Pamoja wa Kigoma (KJP), Shirika la Mitaji la UNCDF liliisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kujenga soko ambalo litakuza mazingira ya biashara katika eneo hilo la mpakani kwa lengo la kuleta mabadiliko katika namna ya uendeshaji biashara unaohusisha kiasi cha wafanyabiashara 3,000, wengi wao wakiwa wanawake.

Justina Amato, ambaye ni mama wa watoto 11 na ni mfanyabiashara katika Soko la Mpakani la Muhange anasema: “Hali katika soko la zamani ilikuwa mbaya hasa wakati wa mvua kwani hakukuwa na mapaa ya kutukinga dhidi ya mvua kubwa.”

Licha ya kuwepo kwa biashara kubwa, bidhaa na huduma ziliuzwa katika eneo la wazi na hakukuwa na mahali pa kuhifadhia mizigo, vyoo, huduma za maji, na huduma nyingine nyingi, mambo yaliyosababisha kuenea kwa magonjwa kama vile kipindupindu katika maeneo ya jirani na soko. Wanawake walikuwa katika mazingira ya kunyanyaswa kijinsia kwa sababu, katika baadhi ya nyakati, walipaswa kufanya biashara huku wamewabeba watoto wao wachanga na kiusafi eneo lilikuwa chafu.

*Inaendelea Ukurasa wa 12*

*Kutoka ukurasa wa 11*

Kwa sababu ya kukosekana kwa majengo ya kudumu katika soko hilo, serikali haikuweza kukusanya ushuru na tozo mbalimbali kwa kiasi kikubwa, hivyo kusababisha fursa za kiuchumi na kibiashara kupotea bure. Aliendelea kusema: “Bidhaa zetu zilikuwa zikiharibika kwani zilizo nyingi ni zile zinazooza kama vile nyanya na matunda, yote haya yalitusababishia hasara kubwa. Soko hili ni la kihistoria kwetu kwani litatusaidia kuhifadhi bidhaa zetu vizuri na kutupunguzia mzigo wa kubeba mizigo yetu kila siku.”

Easter Jacob Jandi ni meneja wa Soko la Mpakani la Muhange, yeye anasema: “Soko ni zaidi ya eneo la kuuza na kununua bidhaa, limekuwa pahali pa burudani ambapo watu hukuana, kunywa, kula na kujadiliana masuala mbalimbali. Kwa soko hili la kisasa, wafanyabiashara huchinji hadi kati ya ng’ombe 10 na 12 za zaidi pamoja na mbuzi na kondoo kila wiki. Tunataraji kuwa biashara itaongezeka mara baada ya mipaka kufunguliwa.”

Akizungumza wakati wa ziara, Ofisa Biashara wa Wilaya ya Kakonko, Bi. Imelda Hokororo, alisema: “Soko humamasiha amani na usalama, halikujengwa tu kwa ajili ya fursa za kazi bali pia kuhamasisha amani na utulivu kati ya mataifa mbalimbali.” Aliongeza kwamba, kabla ya mradi huo, kulikuwa na matukio mengi ya ujambazi, wizi na mauaji yaliyotolewa taarifa kwani watu walikuwa wakifanya biashara kienyeji pasipo kuwa na eneo maalumu. Baada ya kupatikana kwa eneo hilo maalumu, sasa kuna amani kubwa, na wanafanyabiashara wanahakikishiwa usalama wao.

## JAMHURI YA KOREA YATOA MSAADA WA CHUKULA KUSAIDIA WAKIMBIZI

Mapema mwezi Desemba, Ubalozi wa Jamhuri ya Korwa ulikabidhi msaada wa chakula kwa Mpango wa Chakula Duniani (WFP). Tukio hilo lilifanyika katika Bandari ya Dar es Salaam na lilihudhuriwa na Mkuu wa Utendaji katika Ubalozi wa Korea, Bi. Heashin Ahn, Mkurugenzi wa Nchi na Mwakilishi wa WFP, Bi. Sarah Gordon-Gibson na Mkurugenzi Mtendaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Lema.




Mkurugenzi wa Nchi na Mwakilishi wa WFP Bi. Sarah Gordon-Gibson pamoja na Makamu Mkuu wa Ubalozi, Bi. Heashin Ahn na Mkurugenzi wa Bandari, Bw. Elihuruma Lema, wakibeba mifuko yenye nafaka ya Super pamoja na sukari katika Ghala la WFP katika Bandari ya Dar es Salaam. ***PIcha: WFP/Janet Muya***

Bidhaa hizo za chakula zilinunuliwa kwa Dola za Marekani 300,000 zikiwa msaada kwa WFP uliotolewa na Ubalozi wa Korea. WFP ilinunua tani 292 za Nafaka Kuu (Super Cereal)

*Inaendelea Ukurasa wa 13*

*Kutoka ukurasa wa 12*

pamoja na sukari, vyakula vilivyoongezewa virutubisho, ili kutoa msaada katika kazi ya kuhudumia Wakimbizi nchini Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Bi. Gordon-Gibson alisisitiza shukrani zake kwa msaada huo akisema: "chakula hiki kitakuwa msaada mkubwa sana kwa wakimbizi ambao wanategemea kwa asilimia zote msaada wa WFP katika kambi za wakimbizi." Aliongeza kwamba Nafaka Kuu iliyotolewa itakidhi mahitaji yao kwa siku 24, hiyo ikiwa ni pamoja na bidhaa nyingine za chakula—unga wa mahindi wenye virutubisho, kunde, mafuta ya mbogambofa na chumvi.

Akizungumza, Mkuu wa Operesheni katika Ubalozi wa Korea, Bi. Heashin Ahn, alisema kama nchi ambayo zamani ilikuwa ikipokea misaada na hivi sasa inatoa misaada, Korea daima imekuwa ikiongeza msaada wake wa maendeleo na imekuwa ikishirikiana na WFP katika safari yake ya maendeleo. "Nchi yako iko tayari kuondoa njaa kote duniani," alisema Bi. Ahn.

Aliishukuru serikali ya Korea kwa utayari wake wa kutoa mwitikio na katika kuwekeza katika jamii zilizo hatarini zaidi, hasa wanawake na watoto. "Ninafurahi sana




Ofisa wa bandari, akipakia chakula cha msaada katika Ghala la WFP katika Bandari ya Dar es Salaam. Chakula hicho kimenunuliwa kwa fedha zilizotolewa na Korea kwa ajili ya kazi ya kuhudumia wakimbizi. ***Picha: WFP/Janet Muya***

kuona ushirikiano wetu ukizidi kuimarisha na kupanuka, ambapo mchango wa hivi karibuni wa serikali ya Korea wa Dola za Marekanai 300,000 kwa WFP Tanzania utawasaidia sana wakimbizi wanaoishi nchiin Tanzania," alieleza Bi. Ahn.

Alieleza matumaini yake kuwa msaada huo wa chakula utatoa msaada wa kuoakoa uhai kwa wakimbizi nchini Tanania, hasa katika kipindi hiki cha misukosuko ya janga la COVID-19 duniani. "Ninarudia ahadi ya serikali ya Korea katika kuendelea kusaidia maendeleo na kuimarisha maisha ya watu nchini Tanzania na kwa kushirikiana na washirika watu kukabili changamoto mbalimbali nzito za kiutu," alisisitiza.

Mwishoni, Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bw. Elihuruma Lema, alisema Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) imeipa WFP ghala moja kwa ajili ya bidhaa zake za misaada ya kiutu katika Bandari ya Dar es Salaam. "Tumetoa ghala moja maalumu, ambalo sasa linajulikana kama ghala la WFP kwa kutambua umuhimu wa kazi za kiutu zinazofanywa na shirika hili hapa nchini," Bw. Lema alisema akimwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Injinia Deusdedit Kakoko, katika sherehe hizo.

*"Ninarudia ahadi ya serikali ya Korea katika kuendelea kusaidia maendeleo na kuimarisha maisha ya watu nchini Tanzania na kwa kushirikiana na washirika watu kukabili changamoto mbalimbali nzito za kiutu,"*

**Bi. Heashin Ahn, Mkuu wa Operesheni katika Ubalozi wa Korea**

*Inaendelea Ukurasa wa 14*

*Kutoka ukurasa wa 13*




Timu ya WFP katika bandari, Makamu Mkuu wa Ubalozi wa Korea Bi. Heashin Ahn, Mkurugenzi wa Bandari, Bw. Elihuruma Lema, wakiwa katika hafla ya kukabidhi msaada wa chakula katika Bandari ya Dar es Salaam. ***Picha: WFP/Janet Muya***

## KINGA YA MAGONJWA: WATUMISHI WOTE WA MIPAKANI WAWE NA TAHADHARI

Kufuatia ongezeko la utolewaji wa mara kwa mara na dharua za taarifa za tahadhari za magonjwa ya kuambukiza nje ya mipaka na ndani, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (MOHCDGEC) imekuwa ikishirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) na washirika wengine ili kuimarisha ufuatiliaji katika maeneo ya kuingilia nchini ya bandari, viwanja vya ndege na mipaka ya barabara.

Juhudi hizi zimezaa matunda ambapo vituo vyote rasmi 56 vya mipakani vimepatiwa wafanyakazi wa afya na mafunzo zaidi kuhusu udhibiti ili kunoa ujuzi wao pamoja na mbinu za kung'amua mapema katika itifaki ya kuwapokea waingiao nchini yanaendelea.

Katikati ya mwezi Novemba, kwa msaada wa fedha kutoka Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) na WHO ulisaidia kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watumishi wa bandari katika vituo tisa vya mipakani katika Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania vya mikoa ya Rukwa, Katavi, Songwe na Mbeya.

Msaada huo wa uangalizi na mafunzo kwa vitendo viliwajengea uwezo watumishi walio katika vituo vya mipakani ili kubaini, kuwaenga na kuwapa rufaa wote wanaoshukiwa na kuwa na magonjwa na papo hapo kujilinda wenyewe wasiweze kuambukizwa ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Mratibu wa

*Inaendelea Ukurasa wa 15*

*Kutoka ukurasa wa 14*

Afya katika Bandari katika Nyanda za Juu Kusini, Dkt. Deodatus Kilamlya, licha ya mafunzo na kuweka watumishi afya katika bandari, bado Wizara ya Afya ilibaini upungufu katika utekelezaji. "Watumishi wa kada nyingine katika bandari walikuwa wakiacha masuala yote ya afya katika mikono ya maofisa afya pekee, na walikuwa na ulewa finyu kuhusu magonjwa yanayoambukiza kwa kasi," alisema. Mara nyingi eneo la ukaguzi lilikuwa mahali pasipofaa hivyo wageni walichanganyika ovyo kabla mtaalamu hajabaini nani anashukiwa kuwa na ugonjwa na nani hashukiwi.

Wakati wa utoaji msaada huo wa uchunguzi watumishi wa afya na wasio wa afya katika maeneo ya mipakani walijifunza kwa vitendo jinsi ya kutumia mwongozo ulioandaliwa na Wizara ya Afya na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Wahamiaji (IOM) ili kubaini wasafiri ambao wangaliweza kuwa na dalili za ugonjwa.

"Kwa mfano, bawaba anaweza kuona kwamba msafiri fulani anakwenda uani kila baada ya muda mfupi na kuhisi kwamba huyo anasumbuliwa na kuharisha. Mfagizi anaweza kumwomba msafiri huyo aketi katika eneo lililojitenga na kumwita mtumishi kwa hatua zaidi," alisema Dkt. Clara Jones, ofisa wa kituo cha mpakani kutoka Makao Makuu ya Wizara ya Afya ambaye alikuwa miongoni mwa wato mafunzo kwa vitendo.

Kwa kuongezea, maofisa wa bandarini walijifunza na kufanyia marekebisho itifaki za kutenga na kutoa rufaa kwa washukiwa wa ugonjwa, zoezi ambalo walikuwa hawalijui kabla ya mafunzo hayo. "Usalama wa watumishi wetu vilevile ni muhimu kama ilivyo kudhibiti uingizwaji wa ugonjwa wa kuambukza katika mipaka yetu. Kwa hiyo, tunawataka watumishi wote wa mipakani kuunganisha utaratibu wa kila mara wa usafi binafsi katika mienendo yao wawapo kazini na wajishughulishe katika kubaini wasafiri wanaoonekana kuwa na dalili za ugonjwa," alisema Dkt. Jones. WHO pia ilisambaza zana hiyo katika vituo vingine vya mipakani.




Itifaki ya ukaguzi wa udhibiti na kuzuia maambukizi katika vituo vya mipakani ni muhimu sana ili kuzuia mzunguko wa kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza ukiwemo COVID-19. ***Picha/WHO Tanzania***

# MSAADA KWA SERIKALI ILI KUFUFUA UPYA SEKTA YA UTALII

Katika mwitiko wa utayari wa dharura wa Serikali na juhudi zinazoratibiwa na Umoja wa Mataifa katika kukabiliana na COVID-19, Shirika la Mpango wa Maendeleo (UNDP) hivi karibuni lilinunua vifaa tiba ili kuisaidia Serikali ya Zanzibar. Vifaa tiba hivyo vilivyonunuliwa, vikiwa na thamani ya Dola za Marekani 117,441, vinalenga kuimarisha mwitikio wa sekta ya afya dhidi ya COVID-19 na dharura nyingine za kiafya. Vifaa hivyo vinajumuisha Vifaa vya Kujikinga Mtu Binafsi (PPE) zikiwemo mavazi marefu ya kitabibu, barakoa za kitabibu, glavu za uchunguzi na vifaa vya kuhudumia wagonjwa kama Mashine za Kusukuma Hewa katika Chumba cha Dharura, Vifaa vya Kupumulia na Mitungi ya Oksijeni. Vifaa hivyo pia vitachangia katika utekelezaji wa Mwongozo wa Utoaji Huduma (SOPs) kwa COVID-19 ambao utawaongoza watoa huduma kwa watalii, watumishi wa afya na jamii katika kuzingatia kanuni za usalama dhidi ya COVID-19.




Meneja Uendeshaji wa UNDP, Jeremiah Mallongo (kushoto) akikabidhi vifaa tiba kwa Dkt. Juma Mambi (Kulia), ambaye ni Kaimu Mkurugenzi wa Wizara y Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto. ***Picha: Agnes Kenneth/UN Tanzania.***

Kufuatia hatua za hivi karibuni za kulegeza masharti ya safari na kufunguliwa upya kwa maeneo ya utalii huko Zanzibar; UNDP kwa kushirikiana na Tume ya Utalii ya Zanzibar na wadau wengine muhimu katika sekta ya utalii wametengeneza 'Mradi Fungamanishi wa Ufufuaji Utalii na Kujinusuru wa Zanzibar'. Mradi huo unasisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za haraka na fungamanishi katika mwitikio wa kufufua mnyororo wa thamani wa utalii ulio imara na kuaminika huko Zanzibar. Zaidi ya hayo, mradi huo unatarajiwa kuwa na matokeo bora makubwa katika kufufua sekta ya utalii iliyo imara na endelevu zaidi na pia kuimarisha ushindani na ufungamanishaji wa Biashara Ndogo na za Kati (SMEs), wakiwemo wanawake na vijana katika mnyororo wa thamani wa utalii, kwa hiyo kutengeneza nafasi za ajira na hatimaye kuchangia katika kupunguza umaskini nchini.

Sekta ya utalii ya Zanzibar inachangia karibu theluthi moja ya Pato Ghafi lake, asilimia 89 ya mapato yake na ndiyo sekta inayoajiri watu wengi zaidi visiwani humo. Kwa sababu hii, janga la COVID-19 limeangusha kwa kiasi kikubwa sana ukuaji na maendeleo ya mchangiaji mkubwa katika uchumi wa taifa.

# VINARA WA MABADILIKO WANAOPAMBANA NA UKATILI WA KIJINSIA NCHINI TANZANIA



Kala Jeremiah, ambaye ni msanii wa hip hop, mwanaharakati wa kijamii na kinara wa mabadiliko akitoa changamoto dhidi ya Ukatili wa Kijinsia kupitia muziki wake. ***Picha: UNFPA Tanzania***

Rahabu alikuwa na umri wa miaka 17 pale alipopata mimba na kuacha shule, jambo lililokatisha ndoto yake ya kuja kuwa mwalimu. Alirejea kwao katika maji wa Kahama akiwa na miaka 22, baada ya kuachana na mumewe aliyekuwa akimtesa na sasa akiambatana na watoto wawili na alishiriki na kuhitimu katika Mradi wa Wasichana wa Umri wa Balehe ambayo ni programu iliyoanzishwa na Kiota Women's Health and Education (KIWOHEDE) kwa msaada wa UNFPA. Mradi huo unalenga kuwasaidia wasichana waliokatisha masomo yao katika Mkoa wa Shinyanga, kwani mkoa huo ni miongoni mwa mikoa yenye viwango vya juu vya watoto wanaokatisha maomo yao nchini Tanzania.

Leo hii, Rahabu ana kipindi chake cha redio na ni mwanaharakati, akiwaelimisha wanarika wenzake kuhusu umuhimu wa wasichana kuendelea na masomo shuleni. Anatoa changamoto kwa mitazamo waliyo nayo vijana katika jamii yake huko Kahama, akiwasaidia kuhojji imani kwamba mwanamume ana haki ya kutenda ukatili au ikiwa msichana ananyanyaswa, basi alitenda kitu kilichomchokoza mtesi wake.

Rahabu alikuwa mmoja wa vinara 16 waliopata tuzo katika sherehe zilizofanyika mapema Desemba jijini Dar es Salaam katika tukio lililoandaliwa na mashirika ya Women in Law & Development in Africa (WiLDAF) na Coalition Against Gender-Based Violence (MKUKI) kwa ufadhili wa UNFPA na Ubalozi wa Denmark nchini Tanzania kama sehemu ya maadhimisho ya Siku 16 za Uanaharakati wa Kukomesha Ukatili dhidi ya Wanawake.

Vinara hao 16 wa mabadiliko, waliochaguliwa kupitia mchakato wa upendekezwaji, walitokea katika nyanja mbalimbali za maisha na wana hamasa tofauti inayowasukuma kutaka kushiriki katika kukomesha ukatili kwa msingi wa kijinsia lakini wana kitu kinachofanana: wote ni watu wa kawaida wanaofanya mambo ya kipekee, ambapo wanatumia vipawa vyao kukabiliana na ukatili wa kijinsia na wanongezea idadi ya vuguvugu lenye nguvu la kitaifa. Kuanzia kiongozi wa kiroho wa Zanzibar, kijana mwanaharakati wa Shinyanga hadi msanii wa hip hop wa jijini Dar es Salaam ujumbe wa vinara hawa kwa pamoja ni mkubwa na wa wazi kama tukishirikiana, tutafikia katika mabadiliko tunayotaka dunia iliyo sawa zaidi kwa kila mwanamke na kila msichana kokote ulimwenguni.

Licha ya maendeleo yaliyopatikana nchini Tanzania, data zinaonyesha kwamba ukatili dhidi ya wanawake na watot bado uko katika viwango vya juu visivyovumilika; kukabiliana na tatizo kubwa kiasi hiki kunahitaji mwitikio mkubwa vilevile. Kama sehemu ya maadhimisho ya Siku 16,

***Inaendelea Ukurasa wa 18***

*Kutoka ukurasa wa 17*

WiLDAF na MKUKI kwa mara nyingine wakiwa wanafadhiliwa na UNFPA na Ubalozi wa Denmark nchini Tanzania pia waliandaa majadiliano ya kidini huko Zanzibar kwa ajili ya wazee wa kutoka imani zote ambao hawa ni washirika muhimu katika kusukuma maendeleo ya haki za wanawake na wasichana nchini Tanzania. Viongozi wa kidini waliotoa ahadi ya pamoja iliyotiwa saidi ikiahidi kuongeza juhudi za kukomesha ukatili wa kijinsia na vitendo vyote vinavyoleta madhara katika jamii zao.

Tunapoingia mwaka 2021, ambapo tarehe ya ukomo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu mwaka 2030 unazidi kukaribia, UNFPA inaendelea kuazimia kufikia katika ahadi yetu ya dunia na tutaendelea kusaidia juhudi za jamii; kwa kushirikiana, kutumia rasilimali, kufanya zaidi na zaidi na kufanya vizuri zaidi ili kufikia hatma tunayoitaka: dunia iliyo salama zaidi, bora zaidi kwa kila mwanamke na msichana.

## IOM YASHIRIKIANA NA WIZARA YA AFYA KATIKA MWITIKIO KWA COVID-19 NA MASUALA MENGINE YA AFYA YA JAMII

Shirika la Kimataifa la Wahamiaji (IOM) nchini Tanzania, ambalo ni Shirika la Umoja wa Mataifa, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, liliandaa na kutoa mwitikio kwa vitisho vya sasa vinavyosababishwa na ugonjwa wa virusi vya Corona wa 2019 (COVID-19) na Matukio Mengine ya Afya ya Jamii katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Timu ya wataalamu wa ufundi kutoka katika Wizara ya Afya wakipitia Miongozo ya Uendeshaji ya 3. ***Picha: IOM Tanzania***

IOM Tanzania inashirikiana kwa karibu na mashirika ya Umoja wa Mataifa na imetambua Nguzo ya Uongozi katika Maeneo ya Mipaka (PoE) katika Mwitikio wa Umoja wa Mataifa kwa matukio ya masuala ya afya ya jamii nchini. Kwa namna ya kipekee, IOM Tanzania inaongoza katika hatua za kuimarisha ufuatiliaji katika Vituo vya Mipakani, Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi (IPC) na Usafi wa Mazingira na Maji (WASH), licha ya kusaidia Utoaji Taarifa za Hatari na Ushirikishwaji wa Jamii (RCCE) pamoja na Nguzo za Kilojistiki.

IOM ilitekeleza mwitikio dhidi ya COVID-19 kwa kuzingatia malengo maalumu ya Vituo vya Mipakani vya Mpango wa Taifa wa Mwitikio dhidi ya COVID-19 wa Julai, 2020 hadi Juni 2021 katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. IOM iligharimia uandaaji, upitiaji na usambazaji wa 'kanuni za jumla za uendeshaji' (SOPs) kuhusu upimaji wa COVI-19 wakati wa kutoka na kuingia pamoja na Masuala mengine ya Afya ya Jamii katika Vituo vya Mipakani.

*Inaendelea Ukurasa wa 19*

*Kutoka ukurasa wa 18*

Kanuni hizo zinalenga kuimarisha Ufuatiliaji katika Vituo vya Mipakani ili kuzuia na kudhibiti uwezekano wa uingizwaji na upelekaji magonjwa na hatari nyingine za afya ya jamii katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuongezea, IOM iliimarisha uwezo wa watumishi wa Wizara (watumishi 127 wa mipakani na katika bandari) ili kubaini mwitikio wa wagonjwa wa COVID-19 katika Vituo vya Mipakani na hatua za kuimarisha Kuzuia na Kudhibiti Maambukizo, na Usafi wa Mazingira na Maji na kuimarisha Utoaji wa Taarifa za Hatari za Afya ya Jamii na Ushirikishwaji wa Jamii katika njia kuu za mikoa ya Mwanza, Mbeya, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga na Dar es salaam. Kwa namna ya pekee, IOM ilishughulika na watumishi wa afya wa mipakani na bandari katika kuanzisha miitikio ya Utoaji Taarifa za Hatari ya Afya ya Jamii na Ushirikishwaji wa Jamii katika maeneo yao ya kazi ya mipakani na Vituo Maalumu vya Kuingilia. Miitikio ilisambaza taarifa, ushauri wa kuzuia na ushauri kuhusu ni wakati gani na jinsi ya kutafuta huduma za afya kwa wasafiri.

Zaidi ya hayo, IOM ilitoa miongozo ya kiufundi kuhusu ushirikiano katika mipango ya uvukaji mipakani kupitia uwezeshaji wa mikutano ya uratibu inayohusisha nchi




Timu ya wataalamu wa ufundi kutoka katika Wizara ya Afya wakipitia Miongozo ya Uendeshaji ya 4. ***Picha: IOM Tanzania***

nan chi katika kukabiliana na COVID-19 na Matukio Mengine ya Afya ya Jamii. Mwisho, lakini si mwisho kabisa, IOM itato vifaa vya kujikinga, vipima joto visivyo vya kugusa na vifaa vingine vya kufanyia mwitikio na vifaa katika Vituo vya Mipakani na kuwezesha mafunzo kwa vitendo na ya papo kwa papo kwa wafanyakazi walio mstari wa mbele katika Vituo vya Kimkakati vya Mipakani, vituo vya afya katika maeneo ya mipaka, na katika vituo vya rufaa vilivyo kwenye njia kuu.

Hatua hizi za mwitikio zinafadhiliwa kwa fedha kutoka katika Serikali ya Denmark, Sweden na Uingereza. “Maofisa walio Mstari wa Mbele wakiwemo Maofisa wa Afya wa Bandari wanahitaji kupata taarifa sahihi na hatua za haraka za lazima ili kupunguza hatari ya maambukizi na ueneaji wa magonjwa ya kuambukiza,” alisema Mkuu wa Shirika la IOM katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Qasim Sufi.

Shirika la IOM linatumia muundo wa Usimamizi wa Afya, Mpaka na Uingiaji na Utokaji (Health, Border, and Mobility Management (HBMM)) ili kuimarisha utayarifu wa jamii, mwitikio na kuzuia majanga, hasa kipindi hiki ambacho kuna maradhi ya virusi ya COVID-19 na Ebola.

# SIDO: MABADILIKO YA MAHALI BAADA YA UWEKEZAJI



Mwanamke mfanyabiashara kutoka SIDO akianika mbegu za michikichi aki-tumia kikaushia cha jua tayari kwa uchakataji wa mafuta kabla ya msaada wa UNCDF. ***Picha: Mariam Simba/UNCDF Tanzania***

Kihistoria, zao la migazi ni zao la miaka mingi katika Mkoa wa Kigoma. Zao hili hutoa mawese ambayo ni mafuta ya kupikia na kiini cha mbegu yake hutumika katika utengenezaji wa sabuni. Katika Manispaa ya Ujiji Kigoma ndiko kuliko na eneo la viwanda la SIDO, sehemu kubwa ya viini vya mawese vinavyozalishwa Kigoma Vijijini huchakatuliwa SIDO. Inakadiriwa kwamba kilo tatu za mbegu hutoa lita moja ya mafuta. Humchukua mwanamke mchapakazi kati ya siku 4 hadi 7 ili kukausha kilo 660 za mbegu za miwese ili kutoa lita 220 za mafuta, ambapo uzalishaji wa kila siku katika eneo la viwanda ni kuchakata tani 3 kwa siku kwa mashine moja.

Kupitia Mpango wa Pamoja wa Kigoma, Shirika la Mitaji la Umoja wa Matiafa la UNCDF liliisaidia eneo la viwanda la SIDO kubadili kabisa namna ya kukausha mbegu za mawese na uchambuzi kwa kutoa mashine ya kisasa ya kukaushia na kuchambulia mafuta.

Tabitha Charles (42), ambaye ni mama wa watoto 2 anayefanya kazi katika eneo la viwanda la SIDO, alisema: “Nilijiunga SIDO miaka michache iliyopita, kabla ya hapo nilikuwa nikiuza nguo. Changamoto yetu kubwa ilikuwa muda tuliotumia kuanika mazao yetu, ili-chukua hadi siku 5 kwa mazao kukauka kabisa”. Anaongeza: “Siku za karibuni, biashara haikuwa nzuri, kwani hali ya hewa ilikuwa si nzuri, tuli-kuwa na mvua nyingi. Mbegu za miwese haikukauka kwa wakati, ilichukua takribani mwezi mzima. Vilevile ilikuwa vigumu kwetu kupata kuni za kutusaidia katika uchakataji wa mafuta. Nilishindwa kuuza bidhaa zangu kwa wakati jambo lililonifanya kukosa fedha za kulipa karo ya shule ya mtoto wangu.

Tabitha anaamaini kwamba hawatatumia tena muda mrefu kukausha bidhaa kwa kutumia mbinu ya zamani ya jua ambayo haikuwa na ufanisi kwa kulinganisha na mashine za kisasa. “Uwezo wetu wa uzalishaji utaongezeka na tut-aweza kununua mbegu zaidi ili kuzalisha mafuta zaidi.”



Baada ya msaada wa UNCDF, sasa wanawake wafanyabiashara wanatumia mashine za kisasa, ambazo zina kasi zaidi na zina ufanisi zaidi kulinganisha a mashine za kutumia jua. ***Picha / Mariam Simba/UNCDF Tanzania***

## SIKU ZIJAZO ZA UMOJA WA MATAIFA

**February 4 -** Siku ya Kimataifa ya Undugu wa Watu

**February 6 -** Siku ya Kimataifa ya Kutohimili Kabisa Ukeketaji

**February 13 –** Siku ya Redio Duniani

**February 20 -** Siku ya Haki za Kijamii Duniani

## UMOJA WA MATAIFA IMARA KWA DUNIA ILIYO BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA

**Umoja wa Mataifa Tanzania**
+255 22 219 5021
info.untz@one.un.org
Website: tanzania.un.org

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021